MsomihurutzBlog

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**SHULE YA MSINGI *MIWANGANI***
**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA NNE 2026 KISWAHILI - NO.01**
**SEHEMU A: (Alama 20)**

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa na msimamizi, kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi

i. ______________________________________________
ii. ______________________________________________
iii. ______________________________________________
iv. ______________________________________________
v. ______________________________________________

2. Katika kipengele (i) – (x) Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uandike herufi yake kwenye kisanduku ulichopewa

i. Mama hupika chakula."Sentensi hii ipo katika wakati gani?" ___
A. Wa mazoea B. Mtimilifu C. Ujao D. Uliopita ( )

ii. Amelala fofofo, maana ya nahau hii ni ipi?…
A. Amepitiwa na usingizi B. Amelala bila kuamka C. Amelala usingizi mzito D. Amelala kifudifudi ( )

iii. Tunalala usiku na kuamka wakati wa…………
A. Adhuhuri B. Alfajiri C. Jioni B. Mchana ( )

iv. Amina ni mtoto wa dada yake Bakari. Amina atamwitaje Bakari? ___
A. Babu B. Binamu C. Mjomba D. Mpwa ( )

v. Wananchi…….kufika kwenye mkutano.
A. Amewahi B. Ashawahi C. Wamewahi D. Aliwahi ( )

vi. Amevaa miwani. Nahau hii ina maana gani?
A. Amependeza B. Kipofu C. Amelewa D. Anaumwa macho ( )

vii. Malizia usemi huu 'Mwanzo wa ngoma ni.................'
A. Kucheza B. Lele C. Kuimba D. Mzuri ( )

viii. Kipara cha babu chafuka moshi. Tegua kitendawili hiki ___________
B. Ndizi B. Nguo C. Ugali D. Ana kipara ( )

ix. Kamilisha Methali hii 'Jogoo wa shamba..........................'
A.Mtamu B. Hawiki mjini C. Hakosi kamba mguuni D. Hana manyoya ( )

x. Mvumilivu ..............................................................
A. Hachoki B. Huchoka C. Hula mbivu D. Ataumia ( )

**SEHEMU B. (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa kuandika alama sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Kumbe umefika _____umeacha hawajambo_____

(ii) Looh _____ umependeza_____

(iii) Baba analima_____ Mama anapanda mbegu____

(iv) Tunafuga Mbuzi____ Bata na Kuku_____

(v) Ewaaa _______ amesoma vizuri sana ______

4. Panga sentensi zifuatazo kwa mtiririko mzuri kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E katika nafasi uliyopewa.

i. Aliipua na kuchuja chai ikawa tayari ( )

ii. Akamimina maji kwenye sufuria ( )

iii. Alianza kwa kukoka moto ( )

iv. Maji yalipochemka aliweka majani ya chai na sukari ( )

v. Kisha akabandika sufuria jikoni ( )

**SEHEMU C: UFAHAMU (Alama 10)**

5. Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata **kwa kuandika jibu** lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi

Mzee Kayombo anaishi kijiji cha Mtakuja. Mke wa mzee huyo anaitwa Nyamizi, Nyamizi ni mwanamke mkarimu sana. Familia hiyo hujishughulisha na kilimo cha mboga na matunda. Kila mwaka mzee Kayombo huvuna mboga nyingi sana pamoja na matunda. Siku ya Ijumaa hupeleka sokoni mchicha, nyanya, biringanya, bamia na nyanya chungu. Aidha siku ya jumamosi hupeleka pia parachichi, maembe, matango na machungwa.

Mzee Kayombo anawasomesha watoto wake kwa kutumia pesa anazozipata kutokana na kuuza mazao. Kutokana na faida aliyoipata mwaka jana alinunua trekta na mashine ya kusaga.Trekta hiyo inamsaidia katika kilimo na pia humpa pesa kwa kuwa hutumika kuwalimia wanakijiji wenzake.

**MASWALI**

i. Mzee Kayombo anaishi katika kijiji gani?_______________________

ii. Mke wa mzee Kayombo anaitwa nani?_________________________

iii. Familia ya mzee Kayombo hujishughulisha na kilimo cha nini?______________ _____________________

iv. Siku ya jumamosi mzee Kayombo hupeleka sokoni maembe, matango, machungwa na___________________________________

v. Mwaka jana mzee Kayombo alinunua vitu gani? ___________________________

**IFAKARA TOWN COUNCIL**
**MIWANGANI PRIMARY SCHOOL**
**TRIAL EXAMINATION FOR STANDARD IV**
**SUBJECT ; ENGLISH LANGUAGE NO.05**

**SECTION A: 30 MARKS**

**Answer ALL questions in this section**

1. Listen careful to the sentences read in item (i) – (v) and then write them to the space provided

i. ______________________________________________

ii. ______________________________________________

iii. ______________________________________________

iv. ______________________________________________

v. ______________________________________________

2. Choose the correct answer in item (i)- (x) and write its letter in the box provided

i. I am something you use to open or lock a house door ____________

A. torch  C. key  [ ]
B. spoon  D. hammer

ii. Amina rides her________ to school every day

A. bicycle  C. van  [ ]
B. wheelbarrow  D. car

iii. We always cook food in the ______________

A. meat  C. bathroom  [ ]
B. kitchen  D. bedroom

iv. Table, chair, desk, chalk. Which word is different from others?

A. table  C. chalk  [ ]
B. desk  D. furniture

v. A person who sells goods in a shop is called ______________________

A. buyer  C. shopkeeper  [ ]
B. sell  D. fisherman

**vi.** The teacher is _______ us English now.

A. teaching  C. teaches  [ ]
B. taught  D. teach

vii. John _______ a pen and pencil in his bag

A. was  C. have  [ ]
B. has  D. is

viii. We have _______ teachers at school

A. any  C. much  [ ]
B. a lot  D. many

ix. The roof is _______ the classroom

A. under  B. near

C. over [ ] D. in

x. We _______ to Mikumi National Park last holiday

A. go C. going [ ]

B. went D. goes

**3. Complete sentences (i-v) by choosing the correct word provided in the bracket to make sentences meaningful**

i. My brother is a teacher, _________ loves teaching English only.
(he, she, I)

ii. Our school has ____________ computers
(much, many, any)

iii. John __________ Michael are friends
(but, or, and)

iv. I ___________ studying English now
(is, are, am)

v. He __________________ the garden every day
(watering, water, waters)

**SECTION B (10 Marks)**

**Answer ALL questions in this section**

4. Write the correct word for the jumbled letters in the bracket of the following sentences

i. The _____________(ocdrto) examines patients, diagnoses and treat people.

ii. ____________ (itfurs) are like mangoes, apples, oranges and pawpaws.

iii. I went to the ___________(ketmar) with my mother yesterday.

5. Read the following text careful then write the correct form of the verb in brackets in the space provided.

That is Neema. She is (i)_______________(drive) a car. Yesterday she was (ii)____________ (go) to the market to buy some goods such as rice, vegetables, meat, fruits and drinks. When she was on the way to the market, she saw a Monkey which was(iii)_________(eat) a mango. Due to that, Neema was (iv)_________________(look) attentively and laughing to see Monkey eating the mango.

**SECTION C: (10 Marks)**

**6. Read the passage and answer questions that follows**

Last Saturday David and her mother went to hospital to see a doctor. They wait for the bus at bus- stand. After the bus arrived, they interred in and sit near with a driver. At the hospital the nurse used a thermometer to take David's temperature. Then the doctor used X-ray to find out the injured parts of the body. The doctor told David to go to the ward number one, where he should rest for some days. After two days David felt better, therefore he discharged from hospital.

**QUESTIONS**

i. David and her mother wait for a bus at_________________________________

ii. The nurse used a ___________________________to take David's temperature.

iii. The doctor used ________________________ to find out the injured parts of the body.

iv. A ______________ is a place where patients are kept for rest.

v. When patients feel better, they are ___________________ from the hospital.

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**SHULE YA MSINGI *MIWANGANI***

**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA NNE 2025 - NO.05**
**SOMO: HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**
**SEHEMU A: (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) – (x) kwa kuchagua jibu sahihi na kuandika **herufi yake** katika kisanduku ulichopewa.
    i. Haki na wajibu ni maneno yenye dhana tofauti. Tendo lipi kati ya yafuatayo huonesha wajibu wa mtoto ( )
        A. kupata elimu
        B. kulindwa
        C. kupata chakula
        D. kutunza na kuheshimu mali za jamii
    ii. Kutii sheria na kanuni za nchi na jamii ni miongoni mwa_______ ( )
        A. Haki
        B. Wajibu
        C. Heshima
        D. Utii
    iii. Kitendo cha kujikinga dhidi ya mazingira hatarishi kwa kuepuka kuwa katika maeneo hatarishi hujulikana kama ( )
        A. Kujijali
        B. Kujilinda
        C. Kupinga vitendo vya rushwa
        D. Ushirikiano
    iv. Taaluma ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu masalia ya mambo ya kale na utamaduni wa mwanadamu huitwa_____ ( )
        A. Akiolojia
        B. Anthropolojia
        C. Jiolojia
        D. Historia
    v. Maeneo yanayotumiwa kuhifadhi vitu vyenye historia na urithi wa kiasili na kiutamaduni hujulikana kama__________ ( )
        A. Makumbusho
        B. Ukumbi
        C. Stoo
        D. Maktaba
    vi. Vitendo vya rushwa viasababisha kukosekana kwa haki. Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa huitwa_________ ( )
        A. TAWLA
        B. POLISI
        C. TAZARA
        D. TAKUKURU
    vii. Ni kitendo kipi kati ya vifuatavyo vinasababisha uhusiano mwema miongoni mwa watanzania?______ ( )
        A. Kuwa na Imani za jadi
        B. Kugombana
        C. Kushiriki katika sherehe za misiba
        D. Kuwa na ushirikiano na watu wabaya
    viii. Fuvu la binadamu wa kwanza liligunduliwa huko Oldupai. Mwaka gani fuvu hilo liligunduliwa hapa Tanzania? __________________ ( )
        A. 1958
        B. 1959
        C. 1964
        D. 1994

ix. Ipi ni njia ya kale kabisa ya mawasiliano? ________ (  )

A. Ngoma
B. Redio
C. Simu
D. Runinga

x. Hali ya kuipenda na kuilinda nchi yangu inaitwaje?__________ (  )

A. Usaliti
B. Uhaini
C. Uzalendo
D. Ubadhilifu

2. Jibu vipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha fungu **A** na fungu **B** kisha andika herufi ya jibu sahihi kwenye sehemu ya jibu.

| **Na** | **Fungu A** | **Jibu** | **Fungu B** |
|---|---|---|---|
| i. | Zama za mawe za kati | | A. Ngoma na filimbi |
| ii. | Chakula cha asili | | B. Chapati |
| iii. | Ala za asili | | C. Viatu |
| iv. | Watu wenye uhusiano wa kindugu | | D. Kande |
| v. | Ufugaji | | E. Moto |
| | | | F. Jamaa |
| | | | G. Binadamu |
| | | | H. Kutunza wanyama |

3. Jibu vipengele (i) - (v) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyo achwa wazi

i. Nembo inayoashiria umuhimu wa nyaraka husika kwa taifa ni _______________ (Nembo ya taifa, mwenge wa uhuru, wimbowa Taifa )
ii. Mamlaka ya jadi kama vile utemi ilitumiwa na kabila la _____________________ (wachaga, wazanzibari, wahehe.)
iii. Maendeleo yanaweza kutambuliwa katika jamii kwa viashiria vya ongezeko la________________________________________________(watoto, mali, makabila )
iv. Elimu inayohusu matukio yaliyotokea nchini Tanzania tangu mwanzo wa maisha ya watu mpaka leo hujulikana kama___________________________(Historia ya Tanzania, historia, akiolojia)
v. Kabla ya kupata Uhuru wake Nchi ya Tanzania ilitawaliwa na ........................... (wazawa, Dini, Wakoloni)


**SEHEMU B. (Alama18)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Katika kipengele (i) – (iv) onesha vitu vya asili na visivyo vya asili kwa kutumia alama ya *V* katika nafasi uliyopewa

| Namba | Vitu vya asili na visivyo vya asili | Vitu vya Asili | Vitu visivyo vya asili |
|---|---|---|---|
| i. | Mdalasini, iliki na karafuu | | |
| ii. | Malimba, zeze na manyanga | | |
| iii. | Pilau, kababu, sambusa | | |
| iv. | Rede, bao na kuvuta kamba | | |

5. **Tumia picha ifuatayo kujibu swali kipengele cha i hadi v**




i. Taja haki ya mtoto iliyo katika picha na inayotekelezwa shuleni kwako_________________
ii. Ni haki ipi inayomwezesha mtoto kupata maarifa na ujuzi _______________________________
iii. Katika picha kuna vitu vya msingi ambavyo mtoto anastahili kupata na kutendewa. Vitu hivyo vinaitwa_____________________________________
iv. Haki ya msingi inayompa mtoto faragha na usalama dhidi ya vitendo vya ukatili, uonevu, unyanyasaji na udhalilishaji katika pichani ni ____________________________________
v. Katika picha hii mwanafunzi aliyeshika bango na fimbo ana ulemavu gani?___________________

**SEHEMU C. Alama 12**

6. **Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali katika kipengele cha I hadi cha VI**

Tanzania ina urithi adhimu kuhusu shughuli za binadamu wa kale na masalia yake. Mfano Kondoa Irangi Dodoma kuna kumbukumbu za michoro ya mapangoni yenye urithi wa kihistoria unao onesha shughuli za jamii za kale. Oldupai Arusha kuligunguliwa masalia ya fuvu la binadamu wa kale. Huu ni urithi mkubwa kwasababu inaaminika kuwa ndipo alipoishi binadamu wa kwanza duniani. Wageni huja nchini kutembelea maeneo haya ili kujifunza historia ya watu wa kale. Kutokana na wageni hao kutembelea maeneo hayo nchi yetu inapata fedha za kigeni zinazotumika kuleta maendeleo kwa jamii.

**MASWALI**

i. Michoro ya mapangoni katika historia huashiria nini? ________________________________________
ii. Kondoa Irangi ni maarufu kwa kumbukumbu gani za kihistoria?______________________________
iii. Watu gani huja nchini Tanzania kutembelea maeneo ya kihistoria?___________________________
iv. Fuvu la mtu wa kale liligunduliwa katika eneo gani? ____________________________________
v. Wageni wanapotembelea maeneo ya kihistoria, nchi inapata__________________________________
vi. Nini manufaa ya fedha za kigeni zinazopatikana?__________________________________________

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**



**SHULE YA MSINGI *MIWANGANI***



**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA NNE 2025 HISABATI - NO.05**

**SEHEMU A. (Alama 36)**

**Katika swali la 1 – 4 kokotoa na kuandika jibu katika sehemu ya kazi iliyotolewa**

| Na | **Swali** | **Sehemu ya kazi na jibu** |
|---|---|---|
| 1 | i. 5783 + 4057 = | |
| | ii. 948 - 79 | |
| | iii. 19 )‾285 | |
| | iv. 78 x 32 = | |
| | v. $^{2}/_{5}$ x $^{3}/_{7}$ = | |
| | vi. Andika namba ifuatayo kwa kifupi<br>700+ 40 + 9 | |
| 2 | i. Andika kwa tarakimu<br>“Elfu tisa mia nane na nne” | |
| | ii. Andika CMLXXI kwa namba ya kawaida | |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | iii. Andika nafasi ya thamani ya tarakimu iliyopigiwa mstari 63874 | |
| | iv. Andika namba ifuatayo kwa maneno 1010 | |
| | v. Sehemu ipi ndogo kati ya $^{2}/_{6}$ na $^{2}/_{5}$ | |
| 3 | i. Andika namba inayokosekana katika mfulululizo wa namba zifuatazo<br>11, 14 ,17, 20, …………..,26 | |
| | ii. Andika “Kumi na tano nukta tatu tano ” kwa tarakimu | |
| | iii. Badili wiki 12 siku15 kuwa siku | |
| 4 | i. Panga namba zifuatazo kutoka namba ndogo kwenda namba kubwa<br>96 , 41 ,8 ,306 ,64 | |
| | ii. Tafuta eneo la umbo hili<br><br> | |
| | iii. Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo<br><br> | |
| | iv. Mosha aliondoka nyumbani saa 9:15 usiku wa manane kuelekea stendi ya mabasi ya MWANI. Je, muda huo alioondoka huandikwaje kwa mtindo wasaa 24? | |
| | | |
| | **SEHEMU B. (Alama 14)**<br>**Katika swali la 5 na 6 kokotoa na kuandika jibu sahihi sehemu ya kazi iliyotolewa** | |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | i. Mzingo wa mstatili ni sm44 Tafuta upana wake Iwapo urefu wake ni sm 15 | |
| | ii. Shilingi 400 ina senti ngapi? | |
| | iii. Taja idadi ya vipande vya mistari katika mchoro ufuatao   | |
| 6 | i. Chora umbo la Mraba | |
| | ii. Umbo bapa lenye pande nane huitwa…… | |
| | iii. Andika kwa numerali sehemu isiyotiwa kivuli katika umbo lifuatalo  | |
| | iv. Zainabu ana uzani wa kg 3 na gm 460, Sofia ana uzani wa wa kg 1 na gm 630. Nini thamani ya jumla ya uzani kwa wote? | |

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**SHULE YA MSINGI *MIWANGANI***
**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA NNE 2025 SAYANSI - NO.05**

SEHEMU A (Alama 22)

1. Jibu kipengele cha (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika kwenye kisanduku ulichopewa.
   i. Afya bora ni msingi imara katika maisha. Zifuatazo ni kanuni za afya bora ***isipokuwa***______________________ (    )
      A. Kula mlo kamili
      B. Kufanya mazoezi ya viungo
      C. Kwenda kwenye mahoteli ya starehe
      D. Kukaa kwenye mazingira safi
   ii. Vyakula vya kuupa mwili nguvu ni vyenye virutubisho vya wanga au kabohadreti na mafuta. Je ni seti ipi ya vyakula vinavyoupa mwili nguvu? (    )
      A. Nyama, samaki, maziwa na mboga za majani
      B. Mihogo, mtama, mahindi na mchele

C. Maziwa, mboga za majani, maharage na mchele

D. Mihogo, mtama, maziwa na mboga za majani

iii. Alama za onyo zinatoa tahadhari ya tukio la hatari zinazo patikana shuleni au barabarani.Ipi kati ya zifuatazo sio alama ya onyo? (   )

A. Nyanyua kwa uangalifu

B. Hatari

C. Sakafu inayo teleza

D. Usiiingie

iv. Viumbe hai hujumuisha mimea na wanyama. Je tawi lipi la sayansi linajihusisha na viumbe hai ? (   )

A. Baiologia

B. Fizikia

C. Kemia

D. Jiografia

v. Ufuatao ni umuhimu wa sayansi katika maisha ya kila siku kwa binadamu. Upi siyo umuhimu wa sayansi kati ya ufuatao? (   )

A. Inasaidia kujenga maarifa na stadi mbalimbali

B. Inatusaidia kufahamu tamaduni zetu

C. Inatusaidia kutengeneza vitu kama vile sabuni, dawa za meno, mbolea

D. Inasaidia kuendeleza taaluma mbali mbali kama vile ualimu, madawa na uhandisi

2. Jibu kipengele cha (i) – (v) kwa kuoanisha magonjwa toka kifungu **A** na dalili zake toka kifungu **B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi sehemu ya jibu.

| KIFUNGU A | | JIBU | KIFUNGU B |
|---|---|---|---|
| i. | Kutoa sauti kama filimbi au mluzi wakati wa kupumua | | A. UKIMWI |
| ii. | Kuharisha na kutapika mfululizo | | B. Tetekuwanga |
| iii. | Joto kali la mwili na maumivu ya viungo | | C. Kifua kikuu |
| iv. | Husababisha vipele ambavyo hubadilika kama malengelenge | | D. Pumu<br>E. Kipindupindu |
| v. | Kukohoa kwa muda wa wiki mbili au Zaidi | | F. Homa ya matumbo |
| | | | G. Malaria |

3. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| UTONESHAJI, KIZINGITI CHA MGANDO WA MAJI, UVUKIZAJI, MNURURISHO, KIZINGITI CHA MCHEMKO, MPITISHO, MSAFARA, KUAKISI, |

i. __________________Ni usafirishaji wa nishati ya joto katka vitu vigumu kama vile metali

ii. _____________________ ni usafirishaji wa nishati ya joto katika vimiminika kama vile vioevu na gasi

iii. __________________ni usafirishaji wa joto kwenye nafasi tupu kama vile ombwe

iv. Mchakato wa kubadilisha mvuke kuwa hali ya kimiminika inafahamika kama ___________________________________________

v. Kiwango cha jotoridi la nyuzi joto sentigredi 100 au nyuzi joto farenhaiti 212 huitwa ______________________________

vi. ______________ni mwendo wa majimaji kugeuka kua gesi.


**SEHEMU B: (Alama 28)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Umepewa hatua sita (i) – (vi) zilizochanganywa za kufanya uchunguzi wa kisayansi. Panga hatua hizo katika mtiririko mzuri kwa kuzipa herufi A, B, C, D, E na F.

i. Kufanya jaribio na kukusanya data
ii. Kuchambua data
iii. Kuandaa mahitaji ya jaribio
iv. Kubaini tatizo
v. Kubaini dhanio
vi. Kutafsiri matokeo

5. Tumia mchoro hapo chini kujibu maswali




i. Kielelezo hicho kina onesha ogani gani? ________________________________
ii. Sehemu yenye herufi Q inatambua ladha gani? __________________________
iii. Sehemu yenye herufi X inatambua ladha gani? __________________________
iv. Sehemu yenye herufi Y inatambua ladha gani?__________________________
v. Sehemu yenye herufi P inatambua ladha gani? _________________________
vi. Sehemu yenye herufi R inatambua ladha gani?__________________________

6. Jibu maswali yafuatayo kwa kujaza nafasi zilizoacha wazi

i. Kuna makundi mangapi ya viumbe hai? ___________________
ii. Chura yupo kwenye kundi lipi la wanyama?_______________

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**

**SHULE YA MSINGI *MIWANGANI***

**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA NNE 2025 - NO.05**

**SOMO: JIOGRAFIA NA MAZINGIRA NA SANAA NA MICHEZO**

**SEHEMU A: jiografia na mazingira. (alama 26)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Kwa kipengele (i) – (viii) Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uandike katika kisanduku cha kujibia ulichopewa.

i. Jozi ipi ya maneno inawakilisha vitu vya asili katika mazingira? (    )

A. Meza, bustani na mimea    B. Barabara, nyumba na mashamba

C. Milima, mimea na Ardhi  D. Hewa, nyumba na binadamu

ii. Besini, bahari, kilima na milima kwa pamoja hiutwa: (   )

A. Maumbo ya kutengenezwa na binadamu
B. Maumbo makuu ya sura ya nchi
C. Maumbo makuu ya bahari
D. Maeneo makuu ya nchi

iii. Vifuatavyo ni vifaa vinavyotumika kupima urefu katika ramani **isipokuwa** **(   )**

A. Rula
B. Kipande cha karatasi
C. Uzi
D. Mizani

iv. Ni aina gani ya Ramani huonyesha mtawanyiko wa vitu vya asili na vitu vya kutengenezwa na mwanadamu katika uso wa dunia? (   )

A. Ramani za topografia
B. Ramani za kisiasa
C. Ramani za barabara na reli
D. Ramani za thematiki

v. Upi ni mwelekeo wa kivuli chako wakati wa asubuhi? (   )

A. Mashariki
B. Magharibi
C. Kaskazini
D. Kusini

vi. Vifuatavyo ni vifaa vya kufanyia usafi wa mazingira ya ndani ya darasa **isipokuwa;** **(   )**

A. Dekio
B. Sabuni ya maji
C. Kizoleo cha taka
D. Jembe

2. Jibu kipengele (i) – (iv) kwa kuchagua vipengele muhimu vya ramani na ujaze katika sehemu zilizoachwa wazi.

| **Fremu,** | **Skeli,** | **Ufunguo,** | **Kichwa cha ramani,** | **Dira,** | **Chanzo** |
|---|---|---|---|---|---|

i. Huonyesha uhusiano wa umbali uliotumika katika ramani na umbali halisi katika ardhi _______________

ii. Husaidia kutambulisha ramani kwa msomaji kuwa ramani inahusu nini

____________________

iii. Huonyesha mwanzo na mwisho wa ramani______________________________

iv. Huonyesha uelekeo katika ramani ____________________________________


3. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi


i. Upi ni mlima mrefu Zaidi Afrika? __________________________________________

ii. Kifaa kitumikacho kutambua uelekeo, kinaitwaje?___________________________

4. Chunguza ramani ya kata ya Sinza kisha jibu maswali kipengele (i) – (iv) kwa kuandika jibu sahihi sehemu iliyoachwa wazi

**RAMANI YA KATA YA SINZA**






i. Kuna vipengele vingapi vya ramani vimeonyeshwa katika ramani hii___________________

ii. Eneo la Makongo lipo upande gani wa ramani?___________________________________

iii. Kuna barabara ngapi zimekatiza katika mto?_________________________________________

iv. Ni kipengele gani cha ramani hakikuonyeshwa katika ramani hii?_______________________

**SEHEMU B: SANAA NA MICHEZO (Alama 24)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

5. Jibu kipengele cha (i) – (iv) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihihi kisha andika jibu lako kwenye kisanduku ulichopewa.

i. Nini maana ya neno **uigizaji**?
A. Sanaa ya kutengeneza vyombo B. Ni njia ya kuumba vitu C. Ni taaluma ya kufuatisha kitu D. Ni taaluma ya kufinyanga vyungu
( )

ii. Ni kitu gani kinachoweza kutumika kufinyangia vitu mbalimbali?
A. Udongo wa mfinyanzi B.Udongo wa mawemawe C.Udongo tifutifu D. Udongo wa kichanga
( )

iii. Tanzania ina wimbo mzuri wa uzalendo. Mstari unaosema 'Majira yetu haya yangekuwaje sasa' unapatikana katika wimbo upi? A. Tanzania Tanzania B. Mungu ibariki C. Jumuiya yetu D. Tazama ramani

iv. Wanafunzi wa darasa la tatu walichora maumbo ya picha za meza na viti kwa kutumia mistari. Je picha hizo zinaitwaje? A. Picha halisi B. Picha rahisi C. Picha njiti D. Picha bapa
( )

6. Jibu kipengele cha (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku na kuandika katika nafasi uliyopewa.

| Njia ya bapa, kwaya, njia ya pindi, ufinyanzi, hadithi, Kujaza mchanga kwenye chupa |
| --- |

i. Sanaa ya kutengeneza maumbo mbalimbali kwa kutumia udongo wa mfinyanzi_________

ii. Njia ya kufunyanga vifani kama vile mitungi na vyungu vya maua

____________________

iii. Mchezaji wa katikati katika mchezo wa rede anapaswa kufanya nini endapo mpira utarushwa mbali wakati wa mchezo? ________________________________

iv. Aina ya uimbaji inayohusisha waimbaji wengi wakati mmoja _______________

v. Aina ya sanaa za maonesho ambayo hutumia masimulizi kufikisha ujumbe kwa hadhira huitwa______

1. Taja vifaa viwili vya asili vitumikavyo kuchorea picha

i. _________________________________________________________________

ii. _________________________________________________________________

2. Tumia picha ifuatayo kujibu kipengele (i) na (ii) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi



i. Taja jina la mchezo huu __________________________________________

ii. Taja sehemu mbili ambazo mchezo huu unaweza kuchezwa

a. ________________________________________________

b. ________________________________________________